

Je, Mwalimu mzuri ana sifa zipi?



Jishindie kompyuta
ndani!





Hata mimi walimu wangu
wengi walinitenda hayo,
na ndio maana nilimpenda
sana Mwalimu Jonathan.

Aliniheshimu
siku zote.



Aliwahi
kukuchapa
bakora?

Oh! Nilichapwa na
wengine, lakini mwalimu
Jonathan hakuwahi
kutumia kiboko.



Kweli?


Kamwe hakuwahi.
Nilijisikia vizuri siku zote
kwenda kumuona,
nilimwamini!




Safi! Baba
natamani mwalimu
Jonathan angekuwa
anafundisha shulenii
kwetu!



Shule nzuri zina waalimu
wazuri kama
mwalimu Jonathan!




Mwalimu mzuri anaweza
kuwasaidia wanafunzi kukuza
uwezo wao!



Kwahiyo, Mwalimu mzuri ana sifa gani?

Mwalimu mzuri ana sifa nyingi...



Walimu wazuri ni kama
mwalimu wangu.



Anasisitiza uwezo wa
kujieleza...

Jaribu rangi
hii...



...anahimiza udadisi

Kwanini unafikiri mahindi
hayastawi vizuri hapa?



...ananihimiza kuuliza maswali

Kwanini baadhi ya mimea inabadilika rangi na kuwa ya kahawia.



...na kufikiri mwenyewe



Je, ni kwa sababu juu ni kali sana?

Au pengine hakuna maji ya kutosha?

...kujaribu mambo mapya

Oh, vitabu vipy! Sijawahi kuvisoma



na kujifunza kutokana na makosa



Ningejua ningeomba msaada kuvifiki vitabu

Mwalimu wako ni mzuri.




Anaelewa kuwa,
walimu hufanya
mambo mengi zaidi
ya kufundisha.







Kwa sababu tunakuwa waoga na wakimya na tunapoteza mwamko wa kujifunza. Tunaanza kuamini kuwa sisi si wanafunzi wazuri.



Na hilo linaathiri hata maisha yetu ya baadae!

Kama huwezi kujifunza hii namna mpya ya kutunza mahesabu mpaka kufikia wiki ijayo...

Siwezi kujifunza, sina uwezo kabisa!





Mwalimu mzuri anafahamu kwamba kujifunza ni zaidi ya kukariri!



Mwalimu mzuri anatusaidia kujua nini cha kufanya na taarifa...na sio kuzihifadhi tu katika akili zetu.







Mwisho, tunahitaji kutumia
ufahamu wetu



Ninahitaji kiasi gani
cha fedha kila wiki
kama ninataka
kununua ndizi 10
kila siku?

$$\text{Tsh. } 300/- \times 7 = ?$$

Kuchukua tulicho jifunza

Ningekuwa na akiba
ya pesa kiasi gani
kama ningenuna
ndizi 5 kila siku badala
ya 10?

Ningezeitumia pesa kwa
ajili ya nini?





Na tafakari nini cha kufanya na
hiyo pesa

SOKONI



Kujifunza ni mchakato unaohitaji ujuzi.





Anatusaidia kujifunza kutokana na makosa

Unajisikiaje mtu anapoiba vitabu vyako? Utasomaje?



Anatufundisha kufanya maamuzi mazuri



Kwa sababu anajali maendeleo yetu



Na tunapofanya makosa, mwalimu Jimmy anatumia busara kutuelewesha tulichokosea

Stella, utawaomba msamaha wenzako kwa usumbufu, na nitahamisha kiti chako kuja hapa mbele.



Kamwe haogopeshi wala kudhalilisha mtu.

Unazidi kufaulu, insha yako ilikuwa nzuri sana!



Ana sheria na taratibu thabiti

Nategemea nyote mfuate taratibu hizi. Zinaeleweka?



SHERIA ZA DARASANI

- 1.Wahi mapema
- 2.Heshimu wenzako
- 3.Malizia mazoezi ya ziada
- Asante! -

Na tunapovunja sheria, tunajua matokeo yake.

Stella, umechelewesha kazi yako tena. Nafikiri unazifahamu taratibu!

Ndiyo mwalimu, nitabaki baada ya muda wa shule na kuimalizia.



Mwalimu wenu ni mzuri

Ngoja nikwambie
juu ya mwalimu
wangu. Mwalimu
Harriet, ni
mwalimu mzuri
pia!



Mwalimu Harriet ni mwalimu
mzuri kwa sababu
anajivunia shule yetu!



Anajivunia mazingira ya shule



...na kazi yake pia.



...ana uwezo mkubwa na daima
hujiongezea ujuzi,



...anatafuta habari kila mahali,



...na kutumia akili yake kila wakati,



...anatoa mawazo yake na
kujishughulisha darasani,



...kwenye utawala wa shule,



...kwa wazazi pia,



pamoja na jamii nzima!





**Yeye huwa hahamasishi mafanikio tu,
bali juhudhi pia!**

Vizuri sana, Hassan!
Unakumbuka muhula
uliopita ulikuwa wa 22!

Matokeo ya
Mitihani
No. Jumui
11- Bettiini
12- Salima
13- Hassan
14- Tomus
15- Jojo
No. Kato

Ananiheshimu...

Hassan, chukua hiki
kitabu. Ninaamini
utakirudisha.




Anapenda nifaalu...

Kazana! Unaweza!




Na anafurahia mafanikio yangu.



Mwalimu Ahmed ni mfano bora wa kuigwa!


Kazi nzuri sana vijana!



Waalimu wazuri ni mashujaa wetu!!!!



Shule Nzuri ina Waalimu Wazuri!





Je, utafanya nini ili kuwa
mwalimu mzuri?

- Saidia wanafunzi katika muda wa baada ya masomo!
- Wanafunzi wawe vipaumbele vyako!
- Hamasisha maswali!
- Jaribu kutumia mbinu nyingine zaidi ya mihadhara!
- Jifunze mambo mapya!
- Onana na wazazi!
- Wapongeze wanafunzi mara wanapoijahidi!
- Usitumie kiboko!
- Uwe mfano wa kuigwa!
- Shirikisha na jadili na wenzako kuhusu uzoefu wako wa kazi!

Namna ya kutumia kijitabu hiki:

- Orodhesha sifa za mwalimu bora
- Mwambie rafiki yako au mwalimu mwenzio aandae orodha kama hiyo na kisha ifananishe na ya kwako.
- Soma kijitabu hiki pamoja na walimu wengine au wanafunzi shulenii. Kisha jadili jinsi mwalimu bora anapaswa kuwa namna gani.
- Waalimu: someni sehemu moja ya kijitabu hiki kila wiki wakati wa mkutano waalimu kisha jadilini jinsi ya kutekeleza mapendekezo haya.
- Jadilini changamoto zinazoweza kujitekeza katika kufanikisha malengo haya. Kisha andaeni mbinu zinazoweza kusaidia kutatua hizo changamoto.
- Wanafunzi: someni sehemu moja ya kijitabu hiki kila wiki pamoja na rafiki zenu. Kisha jaribuni kubainisha waalimu wazuri katika shule yenu.

Toa maoni, shiriki na jishindie kompyuta!

Msomaji, Serikali yako inataku kukusikia! Shiriki kwa kutuma maoni yako. Mawazo yako yanaweza kuboresha huduma kwa jamii na utawala bora. Pia, hii itakuza ushirikiano kati ya wananchi na Serikali. Maoni yako yatahusiana na **mafunzo** uliyopata kupitia kitabu hiki. Kigezo cha kupata washindi ni ubunifu au wazo jipya.



Zawadi:



Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2012, maoni ya wanafunzi yatakayotumwa kupitia shule zao yatashindanishwa. Maoni kumi bora yatachaguliwa na yatachapishwa kwenye vitabu pamoja na tovuti. Kila shule itakayoshinda itapata kompyuta ndogo mbili (laptops).

Mwisho wa maoni yako weka taarifa zako:



- a) Tarehe
- b) Majina kamili, umri wako na jina la shule/taasisi
- c) Jinsia - Mwanaume/Mwanamke
- d) Anuani (SLP) kamili, makazi (Kata, Wilaya, na Mkoa)
- e) Simu yako na/au Barua pepe (kama unayo).



Unangoja nini! Shiriki basi kwa njia zifuatazo.
Tuma kwa:



- Barua: OGP Ikulu, S.L.P 9120 Dar es Salaam
- Barua pepe: ogp@ikulu.go.tz au opengovtz@gmail.com
- Tovuti: www.wananchi.go.tz

Fikiria. Paza Sauti. Twaweza!

WAALIMU

Viboko
havina
nafasi
hapa!

Mfano
bora zaidi wa
kuigwa!

Kitabu hiki kimeandaliwa na:



Jadili na wenzio ulichojifunza humu
au shiriki mjadala kuitia:



Twaweza_Nisisi



Twaweza Tanzania

www.twaweza.org

www.raisingvoices.org

Hakuna
unyanyasaji
hapa!